




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU



24/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu anakaribisha maombi ya kazi kwa nafasi zifuatazo:-

1.1 MTENDAJI WA KIJIJI III – NAFASI 20

1.1.1 SIFA ZA MWOMBADI

Kuajiriwa wenyewe Elimu ya Kidato cha Nne (IV) AU Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya jamii (Sociology), Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.1.2 MAJUKUMU YA KAZI.

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Serikali katika Kijiji
- Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika
- kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua matatizo/malalamiko na migogoro ya Wananchi katika Kijiji
- Kusimamia Utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji; na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

1.1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS B kwa mwezi

2.0. DEREVA II – NAFASI 4

2.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenyе cheti cha Kidato cha Nne na leseni ya Daraja G, E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na serikali.

2.1.2 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kukagua Gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa Gari.
- Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kweneye safari za kazi.
- Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika Daftari la safari.
- Kufanya usafi wa Gari.
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

2.1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS B kwa mwezi

NB: MASHARITI YA JUMLA.

- Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu
- Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V)
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport Size) na iandikwe jina nyuma.
- **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- Waombaji walistaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 07 /06/ 2022 saa 9.30 Alasiri.
- Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yatumwe kuitia posta kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU,
S.L.P. 74,
MBULU.**


Abubakar A kuuli
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MBULU**


MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA
MBULU